JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA UJENZI

www.mow.go.tz

## TOLEO MAALUM

Septemba, 2023



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa (wanne kulia), Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi Balozi Mha. Aisha Amour (wa pili kulia) pamoja na viongozi wengine akikata utepe kufungua wa Daraja la Msingi lenye urefu wa mita 100 pamoja na barabara za maingilio zenye urefu wa kilomita 1 zilizojengwa kwa kiwango cha lami katika barabara ya Mkoa ya Ulemo (Kitukutu) – Gumanga – Nyahaha (Sibiti) wilayani Mkalama, Mkoani Singida, tarehe 16 Oktoba 2023.





Muonekano wa Daraja la Sibiti (m 82) pamoja na barabara zake za maingilio (km25), mkoani Singida.


## BODI YA WAHARIRI:

**Mwenyekiti**
Segolena Francis

**Wajumbe**
Shukuru Senkondo
Deniza Cyprian
Siti Said
Sandra Kiwia

**Msanifu**
Bolgas Odilo



Wizara ya Ujenzi
S.L.P 2888 Ujenzi
**Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma.**

Simu: +255 26 23244455
Barua pepe: ps@mow.go.tz

# RAIS SAMIA AZIDI KUFUNGUA MIKOA KWA MTANDAO WA BARABARA

Na **Segolena Francis**




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa pamoja na viongozi wengine akiweka Jiwe la ufunguzi wa Daraja la Msingi lenye urefu wa mita 100 pamoja na barabara za maingilio zenye urefu wa kilomita 1 zilizojengwa kwa kiwango cha lami katika barabara ya Mkoa ya Ulemo (Kitukutu) – Gumanga – Nyahaha (Sibiti) wilayani Mkalama, Mkoani Singida, leo tarehe 16 Oktoba 2023. (***Picha na WUJ***)*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuifungua nchi kwa mtandao wa barabara ambapo amezindua daraja la Msingi lenye urefu wa mita 100 na barabara za maingilio zenye urefu wa Kilomita moja kwa kiwango cha lami lililojengwa kwa gharama ya shilingi Bilioni 11.14, leo Oktoba 16, 2023

Kukamilika kwa daraja hilo lililopo Barabara ya Mkoa ya Kitukutu – Gumanga – Nyahala (Sibiti) inayounganisha Mkoa wa Singida, Mwanza na Mara kupitia Daraja la Sibiti lenye urefu wa mita 82 na kilomita 25 kuunga daraja ni juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita za kuboresha na kuunganisha Barabara Kuu na za mikoa Nchi nzima.

Rais Samia amewataka wananchi wa mkoa wa Singida kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuona faida ya daraja hilo lililopo kijiji cha Msingi wilaya ya Mkalama.

Barabara hiyo ni barabara muhimu kwani inaanzia kwenye Barabara kuu ya Singida kwenda Nzega na inaunganisha Barabara itakayojengwa kwa utaratibu wa EPC+F inayoanzia Karatu – Mbulu – Hydom – Sibiti – Lagalo – Maswa yenye urefu wa Kilometa 389 ambazo ni barabara muhimu kiuchumi na kijamii.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa (wanne kulia), Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi Balozi Mha. Aisha Amour (wa pili kulia) pamoja na viongozi wengine akikata utepe kufungua wa Daraja la Msingi lenye urefu wa mita 100 pamoja na barabara za maingilio zenye urefu wa kilomita 1 zilizojengwa kwa kiwango cha lami katika barabara ya Mkoa ya Ulemo (Kitukutu) – Gumanga – Nyahaha (Sibiti) wilayani Mkalama, Mkoani Singida, leo tarehe 16 Oktoba 2023. (**Picha na WUJ**)*

Awali akitoa taarifa ya Mradi huo Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa amesema kuwa maagizo ya Mheshimiwa Rais ya kuweka taa katika madaraja hayo yanatekelezwa na tayari daraja la Msingi limewekwa taa na madaraja mengine yatawekwa taa mara baada ya Mkandarasi kukamilisha ujenzi.

Bashungwa amemshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha za miradi hiyo pamoja na miradi mingine aliyoelekeza itekelezwe kwani inazidi kuunganisha mikoa ya Kanda ya Ziwa, mikoa ya Kati na kanda ya Kaskazini na kusema kuwa Rais ni mtu wa kazi na anatekeleza ahadi zake




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Wananchi wa kijiji cha Msingi wilayani Mkalama wakati wa hafla ya Ufunguzi wa Daraja la Msingi lenye urefu wa mita 100 pamoja na barabara za maingilio zenye urefu wa kilomita 1 zilizojengwa kwa kiwango cha lami katika barabara ya Mkoa ya Ulemo (Kitukutu) – Gumanga – Nyahaha (Sibiti) mara baada ya kuweka Jiwe la ufunguzi wa Daraja hilo Mkoani Singida, leo tarehe 16 Oktoba 2023.*



**PICHANI:** *Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa wakati akitoa Maelezo kuhusu Daraja la Msingi lenye urefu wa mita 100 pamoja na barabara za maingilio zenye urefu wa kilomita 1 zilizojengwa kwa kiwango cha lami katika barabara ya Mkoa ya Ulemo (Kitukutu) – Gumanga – Nyahaha (Sibiti) kabla ya kuweka Jiwe la ufunguzi wa Daraja hilo, wilayani Mkalama, Mkoani Singida, leo tarehe 16 Oktoba 2023. (***Picha na WUJ***)*



*Mwonekano wa Daraja la Msingi lenye urefu wa mita 100 pamoja na barabara za maingilio zenye urefu wa kilomita 1 zilizojengwa kwa kiwango cha lami lililopo katika barabara ya Mkoa ya Ulemo (Kitukutu) – Gumanga – Nyahaha (Sibiti) wilayani Mkalama, mkoani Singida ambalo Ujenzi wake umegharimu jumla ya ni Shilingi Bilioni 11.2, leo tarehe 16 Oktoba 2023. (***Picha na WUJ***)*



**PICHANI:** *Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa na viongozi wengine akiweka Jiwe la Msingi la Ujenzi wa barabara ya Makongolosi – Rungwa – Itigi - Mkiwa, Sehemu Noranga – Itigi - Mkiwa (Kilometa 56.9) inayojengwa kwa kiwango cha lami, leo tarehe 15 Oktoba 2023 Itigi Singida. (***Picha na WUJ***)*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa katika Uwanja wa Police Square, Itigi Mkoani Singida mara baada ya kuweka Jiwe la Msingi la Ujenzi wa barabara ya Makongolosi – Rungwa – Itigi - Mkiwa, Sehemu Noranga – Itigi - Mkiwa (Kilometa 56.9) inayojengwa kwa kiwango cha lami, leo tarehe 15 Oktoba 2023*

# MAKAMU WA RAIS DKT. MPANGO AITAKA TBA KUJITEGEMEA

Na **Deniza Cyprian**



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa jengo la makazi la kibiashara lililopo katika makutano ya barabara ya Kinana na Afrika Mashariki eneo la Sekei, jijini Arusha.*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango amefungua jengo la makazi la kibiashara na kusisitiza kwamba Serikali itaendelea kuziwezesha Taasisi zake kuwa na miradi mikubwa itakayoziwezesha kujitegemea.

Akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa jengo la makazi la kibiashara lililo sekei jijini Arusha Dkt. Mpango amesema Serikali imeiruhusu Wakala wa Majengo Nchini (TBA) kushirkiana na sekta binafsi kwa ubia ili kuiwezesha kutekekeza miradi ya kimkakati na itakayoleta tija haraka na hivyo kupunguza utegemezi wake kwa Serikali.

"Nawapongeza kwa ujenzi wa jengo zuri la kisasa, endeleeni na mpango wa kujenga majengo ya aina hii katika maeneo mbalimbali ya kimkakati yatakyowezesha kuhudumia kaya nyingi na zingatieni uhifadhi wa mazingira na kwa kupanda miti na maua na kuweka mifumo mizuri ya kuondosha takataka' amesema Dkt. Mpango.

Dkt. Mpango ameitaka TBA kufanya uwekezaji wenye tija katika maeneo yake na kuhakikisha wapangaji wa majengo yake wanalipa kodi kwa wakati.

Ameitaka Wizara ya Uwekezaji kuhakikisha inaweka msukumo kwenye ujenzi wa viwanda vya vifaa vya ujenzi ili kupunguza gharama za ujenzi hivyo kuwezesha Serikali kufikia lengo la ujenzi wa nyumba nyingi zitakazokidhi mahitaji ya ongezeko la idadi ya watu.

"Serikali imedhamiria kukuza sekta ya nyumba ili ichangie pato la Taif ana hivyo kukuza uchumi' amesisitiza Dkt. Mpango.




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, akipokea tuzo ya heshima kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Arch. Daud Kondoro wakati wa hafla ya ufunguzi wa jengo la makazi la kibiashara lililopo katika makutano ya barabara ya Kinana na Afrika Mashariki eneo la Sekei, jijini Arusha.*



*Muonekano wa Jengo la Makazi la Kibiashara la Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), lenye sakafu 11 na uwezo wa kuhudumia kaya 22, lililopo katika makutano ya barabara ya Kinana na Afrika Mashariki eneo la Sekei, jijini Arusha.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango pamoja na viongozi wengine wa Serikali wakifungua pazia kuashiria ufunguzi wa jengo la makazi la kibiashara lililopo katika makutano ya barabara ya Kinana na Afrika Mashariki eneo la Sekei, jijini Arusha.*




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, akipata maelezo kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Arch. Daud Kondoro wakati wa hafla ya ufunguzi wa jengo la makazi la kibiashara lililopo katika makutano ya barabara ya Kinana na Afrika Mashariki eneo la Sekei jijini Arusha.*

# MAJALIWA AWATAKA ERB KUJA NA MKAKATI WA KUWAINUA WAHANDISI WA NDANI

Na **Shukuru Senkondo**



*Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akiwahutubia wahandisi na viongozi mbalimbali wa Wizara ya Ujenzi wakati wa Mkutano wa 20 wa Wahandisi uliofanyika Mlimani City, Dar es Salaam.*

Waziri mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ameitaka Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), kupeleka mapendekezo Serikalini ya namna ya kuwatumia wahandisi wa ndani katika miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali ili kuwapa fursa ya kukua na kuongeza uzoefu katika miradi hiyo.

Akifungua mkutano wa 20 wa siku ya wahandisi nchini Waziri Mkuu Majaliwa amesema dhamira ya Serikali ni kuona sekta ya uhandisi nchini inakuwa na kuwapa fursa wahandisi wazawa ambao mchango wao katika maendeleo ya nchi ni mkubwa.

"Hakikisheni mnaungana, mnakopa katika benki ili muwe na nguvu ya kutekeleza miradi mingi inayoendelea kutekelezwa na serikali hususan ya ujenzi wa miundombinu", amesema Mhe. Majaliwa.

Aidha, amewataka wahandisi hao kutumia fursa kwa kuwa wabunifu na kuendana na teknolojia ili nchi isibaki nyuma katika kuchagiza maendeleo katika sekta ya miundombinu, sayansi na teknolojia.

"Tumieni vizuri siku hizi mbili kufanya uchambuzi wa kina na kuja na mapendekezo yatakayowezesha Serikali kutatua changamoto zinazowakabili kwa kuwawezesha kushiriki katika ujenzi wa miradi mikubwa inayoendelea nchini", amesema Waziri Mkuu Majaliwa.

Ameutaka Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), kuwapatia wazawa miradi midogo inayoendelea ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza miradi mikubwa katika siku zijazo kama inavyofanya TANROADS.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Ujenzi Mhandisi, Godfrey Kasekenya amesema Serikali inatambua umuhimu wa wahandisi katika kuleta maendeleo ya taifa ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga shilingi milioni 726, kwaajili ya mradi wa SEAP – mradi ambapo umelenga kuwajengea wahitimu wa fani hiyo uzoefu.



Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya akizungumza na wahandisi wakati wa Mkutano wa 20 wa Wahandisi uliofanyika Mlimani City, Dar es Salaam jana.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akisisitiza jambo alipotembelea banda la Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) alipotembelea banda lao kwenye Mkutano wa 20 wa Wahandisi uliofanyika Mlimani City, Dar es Salaam jana. Wa pili kushoto ni Mtendaji Mkuu wa wakala hiyo, Mhandisi Victor Seff.

# BIL.400/- KUKARABATI BARABARA MTWARA - MINGOYO - MASASI

Na **Deniza Cyprian**



*Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa akizungumza na wananchi waliofika katika mkutano wa hadhara wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika Uwanja wa Mitwero mkoani Lindi tarehe 19 Septemba, 2023.*

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amesema shilingi bilioni 400 zitatumika katika ukarabati wa Barabara ya Mtwara-Mingoyo-Masasi kupitia majadiliano yaliyofanywa kati ya Serikali na Benki ya Dunia (WB).

Pia, ampongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa barabara inayounganisha vipande kutoka Masasi- Nachingwea - Liwale (km 175).

Waziri Bashungwa aliyasema hayo leo katika mkutano wa hadhara wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na wananchi uliofanyika katika Uwanja wa Mitwero mkoani Lindi wakati akitoa salamu na kueleza utekelezaji wa miradi ya kimaendeleo mkoani humo.

Waziri Bashungwa alisema pamoja na Serikali kuendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hiyo lakini Rais Dk. Samia Suluhu Hassan tayari ameridhia kusainiwa kwa barabara hiyo.

“Rais Samia Suluhu Hassan umetuelekeza Wizara ya Ujenzi hata kabla fedha wakati tunaendelea kuzitafuta, umeelekeza kwa namna ambavyo unawajali wananchi wa mikoa hii miwili kwamba tusaini huku ukiendelea kupambana kutafuta fedha ya barabara hii ambayo italeta mageuzi makubwa ya kiuchumi kwa Mkoa wa Lindi na Mtwara”, alisema Bashungwa.

Ameongeza kuwa Mhe. Rais ameelekeza mkandarasi wa barabara ya Nachingwea - Ruangwa - Nanganga yenye urefu wa kilometa 53.2 ambayo tayari ujenzi wake umefikia asilimia 41 aendelee na ujenzi wa barabara hiyo hadi Nachingwea ambapo itakuwa na jumla ya urefu wa kilometa 106.

Kuhusu Barabara ya Nangurukuru - Liwale (km 230) Waziri Bashungwa alisema tayari Serikali imetenga fedha za kuanza ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 72 kuanzia Liwale hadi Choya.

“Mhe. Rais kama hiyo haitoshi kipo kipande cha Barabara ya Ruangwa-Namichiga kilometa 20 ambacho kwa sasa kipo kwenye mipango ya kuwekwa lami kupitia mradi wa RISE, sasa ukiona mahaba na Watanzania wakijitokeza kwa wingi unakopita ni kwamba wewe ni Rais wa vitendo na wanaona kazi kubwa ya Serikali unayoiongoza”, alisema Bashungwa.

# WAZIRI BASHUNGWA AITAKA TEMESA KUJIENDESHA KIBIASHARA

Na **Segolena Francis**



*Waziri wa Ujenzi, Mhe. Innocent Bashungwa (katikati), akizungumza na Menejimenti ya Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) katika kikao kazi kati ya Menejimenti ya Wakala huo na Waziri huyo, jijini Dodoma. Kushoto ni Katibu Mkuu Wizara ya ujenzi Mha, Balozi Aisha Amour na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Lazaro Kilahala,*

Waziri wa Ujenzi Mhe. Innocent Bashungwa, ameutaka Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) kuja na mikakati itakayouwezesha Wakala huo kufanya kazi kibiashara ili kuleta tija katika utendaji kazi wake.

Akizungumza mara baada ya kukutana na Menejimenti ya wakala huo Mhe Bashungwa amesema huu sio wakati wa TEMESA kulalamika na kusononeka, ni wakati wa kujali wateja na kushindana katika soko ili kupata wateja wengi na kuhudumia sehemu kubwa ya jamii kwenye upande wa umeme, eletroniki, mitambo uendeshaji wa vivuko na utengenezaji wa magari.

‘’Namshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapa fedha za kutosha za kusimamia miradi yenu, hivyo hakikisheni mnazitumia fedha hizo kwa uaminifu na uadilifu na kuhakikisha miradi ya ujenzi mnayoendelea nayo hususani ya vivuko na huduma za ufundi wa umeme na magari inakamilika kwa wakati,’’amesema Mhe. Bashungwa.

Waziri huyo wa Ujenzi amewataka wafanyakazi wote wa TEMESA kufanya kazi kwa mtazamo chanya utakaovutia jamii kubwa ya Watanzania kutumia huduma za TEMESA ambazo zitakuwa bora, za uhakika na za kuaminika badala ya kwenda kupata huduma hizo kwenye taasisi zingine.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Ujenzi, Mhandisi Balozi Aisha Amour, amemhakikishia Waziri wa Ujenzi kuwa TEMESA iko kwenye mkakati wa mabadiliko katika utendaji na ukusanyaji wa mapato ili kuhakikisha mapato yote yanayopatikana yanakusanywa kwa wakati.

Mtendaji Mkuu wa TEMESA Lazaro Kilahala, amesema kuwa maelekezo yote na miongozo iliyotolewa na Wizara itafanyiwa kazi na kuelekezwa kwa watumishi wote wa Wakala huo nchini.

Waziri Bashungwa alikua katika ziara ya kukutana na Menementi ya TEMESA ikiwa ni mara ya kwanza tangu alipoteuliwa na Mhe Rasi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwa Waziri wa Ujenzi.

# UPEMBUZI YAKINIFU WA BARABARA YA KARATU-MANGOLA-SIBITI WAKAMILIKA

Na **Deniza Cyprian**



*Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, akijibu swali Bungeni jijini Dodoma, leo katika kikao cha Tisa cha mkutano wa 12.*

Serikali imesema imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya njia panda (Karatu) – Mangola – Matala – Sibiti River hadi Lalago yenye urefu wa kilometa 328 inayojulikana kama "Eyasi Route".

Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya, amesema hayo bungeni leo wakati akijibu swali la Mheshimiwa Daniel Tlemai Awack, Mbunge wa Karatu, aliyetaka kujua maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo.

Naibu Waziri Kasekenya ameliambia bunge kuwa Sehemu ya kuanzia Sibiti River hadi Lalago yenye urefu wa kilometa 121 imejumuishwa kwenye mradi wa EPC +F kupitia barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389) ambayo mkataba wake wa ujenzi umeshasainiwa.

Amesema sehemu iliyobaki ya Njia Panda ya (Karatu) – Mangola hadi Matala (km 137), Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Aidha, Eng. Kasekenya amesema kuwa Serikali bado inatambua umuhimu wa barabara ya Liwale hadi Mahenge kwa wananchi kwa kuwa inapitika katika Hifadhi ya Mwalimu Nyerere.

"Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii kiulinzi na kijamii na barabara hii kuunganisha Mikoa ya Lindi na Morogoro, imetenga jumla ya Shilingi milioni 143.04 kwa ajili ya kazi za Upembuzi Yakinifu wa Awali", amesema Eng. Kasekenya.

Ameongeza kuwa Kazi ya Upembuzi Yakinifu wa Awali itakapokamilika katika Barabara hiyo inayopita katika Hifadhi ya Mbuga ya Wanyama ya Selous itaonesha iwapo mradi unakidhi vigezo vya uhifadhi mazingira ili kuwezesha kujengwa.

Mheshimiwa Kasekenya alikuwa akijibu hayo katika mkutano wa 12 kikao cha Tisa cha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililoahirishwa leo.

# RAIS DKT. SAMIA YUPO 'SERIOUS' NA UJENZI WA BARABARA NCHINI

Na **Segolena Francis**



*Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa akizungumza na wananchi waliofika katika mkutano wa hadhara wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, eneo la Ikwiriri Mkoani Pwani tarehe 20 Septemba, 2023.*

Waziri wa Ujenzi Mhe. Innocent Bashungwa amesema ujenzi wa miundombinu ya barabara nchini unafanyika kwa umakini na viwango vya ubora chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Waziri Bashungwa ameyasema hayo leo Septemba 20, 2023 mbele ya wananchi wa Ikwiriri mkoani Pwani ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa mikoa ya Kusini.

"Sisi kazi yetu ni kutekeleza yale ambayo Mhe. Rais ametuagiza, kwenye maelekezo uliyotupatia ya utiaji saini mikataba mbalimbali ambayo inakaribia trilioni 2 hata TARURA watakuwepo kuonesha namna Serikali yako ilivyojipanga katika ujenzi wa barabara", amesema Mhe. Bashungwa.

Katika hatua nyingine Waziri Bashungwa amesema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameagiza upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Barabara ya Mabasi yaendayo haraka kutoka Mbagala - Vikindu ufanyike haraka ili utaratibu wa kuanza ujenzi uanze mara moja.

"Mhe. Rais BRT kutoka Mbagala rangi tatu hadi vikindu umetuelekeza usanifu ufanyike haraka ili barabara hiyo na njia nne ije mpaka Vikindu ili wananchi wa mkoa wa hapa Pwani na Rufiji waweze kuingia Dar es Salaam kwa wepesi na kutoka kwa wepesi"- amesema Mhe. Bashungwa.

Naye Mbunge wa Rufiji ambaye pia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe. Mohammed Mchengerwa amesema Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameridhia kutoa kiasi cha Shilingi Bilioni 75 kuanza ujenzi wa barabara ya Nyamwage - Utete yenye urefu wa kilometa 37 na tayari wakandarasi wanaendelea na ujenzi wa barabara hiyo.

"Naomba nichukue nafasi hii kukushukuru Mhe. Rais kwa kuridhia kujenga barabara ya Ikwiriri- Mkongo kwa kiwango cha lami na tayari mkandarasi yupo site amekwishaanza kujenga daraja la mbambe na barabara itakayotoka mbambe kuja hapa Ikwiriri mjini"- ameongeza Mhe. Mchengerwa.

# TANROADS YAAGIZWA KUBAINISHA MAENEO YOTE KOROFI YA BARABARA NCHINI

Na **Siti said**



*Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa akijibu maswali ya wabunge katika Bunge la 12, jijini Dodoma.*

Waziri wa Ujenzi, Mhe. Innocent Bashungwa, amewaagiza Mameneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mikoa yote kufanya Upembuzi yakinifu na kubaini maeneo yote korofi ya Barabara na kuyawasilisha Wizarani ili yaweze kupewa kipaumbele wakati wa kuandaa bajeti.

Bashungwa, ameyasema hayo leo Bungeni jijini Dodoma wakati akijibu Swali la nyongeza la Mbunge wa Jimbo la Tandahimba, Mhe.Katani Ahmed aliyetaka kujua lini Serikali itatenga fedha ya dharura kujenga kipande cha Barabara ya Nguja - Mkwiti - Tandahimba yenye maeneo Korofi.

"Nitumie nafasi hii kuwaelekeza Mameneja wa TANROADS mikoa yote kuangalia maeneo yote korofi na kufanya Upembuzi yakinifu na kuyawasilisha Wizarani ili yapewe kipaumbele wakati wa kuandaa bajeti" amesema Bashungwa.

Aidha, Mbunge wa Tandahimba, Mhe. Katani Ahmed alitaka kujua Je, ni lini ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara kutoka Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala hadi Masasi utaanza, ambayo ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi 2020 na ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Wakati akijibu swali hilo, Bashungwa amesema ujenzi wa barabara ya Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala – Masasi yenye urefu wa kilometa 210 unatekelezwa kwa awamu ambapo ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Mtwara – Mnivata (km 50) umekamilika kwa kutumia fedha za ndani.

Bashungwa amesema kuwa sehemu ya barabara ya Mnivata – Newala - Masasi (km 160) chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imesainiwa tarehe 21 Juni, 2023 kwa sehemu za Mnivata – Mitesa (km 100) na Mitesa – Masasi (km 60) pamoja na ujenzi wa Daraja la Mwiti, kwa sasa Makandarasi wa sehemu zote mbili wapo katika hatua za maandalizi ya kuanza ujenzi.

# BASHUNGWA: BARABARA APP SULUHU LA MIUNDOMBINU YA BARABARA

Na **Theresia Mwami**




*Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, akizunguma na menejimenti ya Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), mara baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Bodi hiyo iliyo chini ya Wizara ya Ujenzi, jijini Dodoma Septemba 27, 2023.*

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amewataka wananchi kutoa taarifa za hali ya barabara nchini kupitia mfumo wa kieletroniki wa 'Barabara App' ili hatua za haraka kwa barabara zinazohitaji matengenezo ziweze kuchukuliwa.

Amesema kupitia mfumo huo, watumiaji wa barabara wanaweza kushiriki katika kusimamia miundombinu ya barabara katika maeneo wanayoishi au kupita kwa kutuma taarifa muhimu za hali ya barabara katika Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), ambapo Bodi hiyo itawasilisha mahala husika katika Taasisi ya Wakala ya Barabara Nchini (TANROADS) na Wakala ya Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

Ametaja miongoni mwa taarifa hizo ikiwemo barabara kujifunga, daraja au kalvati kubomoka/ kuzolewa na mafuriko, mashimo hatarishi barabarani, kazi kufanyika chini ya kiwango, mitaro kuziba na hujuma zozote zinazofanyika katika miundombinu ya barabara.

Waziri Bashungwa ameyasema hayo Septemba 27, 2023 jijini Dodoma wakati akihitimisha ziara yake katika Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB) ambapo Waziri huyo alipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Bodi hiyo.

"Niwaombe watanzania kutumia mfumo huu unaomwezesha mwananchi kutoa taarifa ya hali ya miundombinu ya barabara yenye changamoto, au hujuma yoyote maeneo anayoishi", amefafanua Bashungwa.

Bashungwa ameongeza kuwa lengo la kuwa na mfumo huo ni kuipunguzia Serikali gharama kubwa za matengenezo ambayo ingeia kutokana na uchelewaji wa matengenezo hayo.

Aidha, Bashungwa amesema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imejipanga vyema kuhakikisha Taasisi ya Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) inayosimamia barabara kuu na za mikoa na ile ya Wakala ya Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), inayosimamia barabara za Halmashauri/ Wilaya wanajipambanua zaidi katika kuhudumia barabara zote nchini.

Amewataka watanzania kuwa na imani na taasisi hizo katika kuhudumia na kusimamia mtandao a barabara nchini kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu yao.

"Ningependa kuwajulisha watanzania kuwa huko nyuma kulikuwa na maombi makubwa ya barabara ambazo zipo kwenye wilaya zetu ili zipandishwe hadhi kuja TANROADS, lakini hivi sasa hilo hitaji ni kama limeisha kwasababu TARURA imekwisha jengewa uwezo na kuimarishwa mfuko wake", amefafanua Bashungwa.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Bodi hiyo, Kaimu Mtendaji wa RFB Eng. Rashid Kalimbaga, ameeleza kuwa mbali na mfumo wa kieletroniki wa kufuatilia barabara Bodi imeimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha kwa lengo la kuongeza ufanisi na kuzuia matumizi mabaya ya fedha.

Ameongeza kuwa kuimarika kwa mifumo hiyo kutaziba mianya ya uvujaji wa mapato pamoja na uchakachuaji katika ujenzi na matengenezo ya barabara.



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Balozi Eng. Aisha Amour, akizungumza mbele ya Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa wakati wa uwasilishwaji wa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB), jijini Dodoma Septemba 27, 2023.*



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI
BODI YA MFUKO WA BARABARA

# TOA TAARIFA YA HALI YA BARABARA SASA

## *Ni Rahisi*

1. Fungua "Play Store" au "App Store"
2. Tafuta neno "Barabara"
3. Bonyeza kitufe cha "Install" mpaka ifike 100%
4. Bonyeza kitufe cha "Open" fuata maelekezo ya kutoa taarifa ya hali ya barabara

Google Play

Available on the App Store




**Barua pepe:** info@roadsfund.go.tz
**Tovuti:** www.roadsfund.go.tz

@rfb_tz

# SERIKALI KUJENGA MADARAJA YA MALAGARASI-ILAGALA NA LUGONESI

Na **Shukuru Senkondo**



*Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya akisisitiza jambo kwa Mbunge wa Kigoma Kusini Mhe. Nashon Bidyanguze (kushoto), Meneja wa TANROADS mkoa wa Kigoma Eng. Narcis Choma na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kigoma Kusini Mhe. Mateso Jackson (mwenye suti nyeusi), alipokagua barabara ya Simbo-Kalya KM 235 mkoani Kigoma.*

Serikali imesema katika mkakati wake wa kuufungua mwambao wa ziwa Tanganyika itajenga madaraja ya Malagarasi-Ilagala na Lugonesi ili kuunganisha kwa njia fupi mikoa ya Kigoma na Katavi na hivyo kuchochea shughuli za uzalishaji wa mazao, uvuvi na ufugaji katika maeneo hayo.

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya alipokagua maendeleo ya uanzishwaji wa barabara mpya ya Simbo-Kalya KM 235 inayopita pembezoni mwa ziwa Tanganyika na kuunganisha mikoa ya Kigoma na Katavi.

"Hadi mwezi Disemba tutahakikisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika ili kazi ya ujenzi wa madaraja haya mawili pamoja na barabara unganishi zenye zaidi ya KM 7 uanze", amesema Eng. Kasekenya.

Amebainisha kuwa wakati Serikali ikitafuta fedha za kuijenga barabara hiyo itahakikisha maeneo korofi yanajengwa kwa kiwango cha zege ili kuiwezesha kupitika kipindi chote cha mwaka.

Naibu Waziri huyo amewapongeza mameneja wa Wakala wa Barabara TANROADS mkoa wa Kigoma na Katavi kwa kazi za kuanzisha barabara mpya katika maeneo yao ili kurahisisha huduma ya usafiri ikiwa ni pamoja na kuunganisha barabara na bandari za ziwa Tanganyika.

"Kwa kweli nimeridhika kwa bidii na ubunifu wa mameneja hawa ya kuanzisha barabara mpya huu ni ubunifu mzuri na Serikali itatafuta fedha ili barabara hizi zijengwe kwa lami", amesisitiza Eng. Kasekenya.

Naibu Waziri huyo amewataka wananchi wa mikoa ya Kigoma na Katavi kulinda miundombinu ya barabara ili idumu kwa muda mrefu na kuepusha hasara kwa serikali na ukosefu wa usalama kwa wananchi wanaotumia barabara hizo.

"Acheni kuchimba mchanga barabarani na chini ya madaraja, epukeni wizi wa alama za barabarani na taa, eleweni Serikali inatumia gharama kubwa kujenga miundombinu hii hivyo kuilinda ni kuiunga mkono Serikali", amesisitiza Eng. Kasekenya.

Meneja wa (TANROADS), mkoa wa Kigoma Eng. Narcis Choma amesema ujenzi wa barabara na madaraja utaendana na utoaji elimu ya uzalendo kwa wananchi namna ya kuilinda miundombinu kwa maslahi mapana ya taifa.

# BASHUNGWA AAGIZA TATHIMINI UJENZI WA MIZANI

Na **Deniza Cyprian**



*Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, akitizama mfumo wa kupima uzito wa magari katika Mzani wa kupima uzito wa magari wa Uyole uliopo mwanzoni mwa barabara ya Uyole - Kasumulu (mpakani mwa Tanzania na Malawi), mkoani Mbeya.*

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, ameagiza wataalam wa wizara hiyo kufanya tathimini ya mizani zote nchini na kuangalia bajeti ya kuweka mizani ya kigitali ya kupima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (weigh in motion), ili iwe katika vipaumbele vya Serikali katika mizani zote ambazo hazijafungwa mfumo huo na zile zitakazojengwa.

Bashungwa ameyasema hayo Oktoba 3, 2023 mkoani Mbeya wakati akikagua kazi zinazoendelea katika mzani wa Uyole uliopo mwanzoni mwa barabara ya Uyole - Kasumulu (mpakani mwa Tanzania na Malawi).
"Dhamira ya Serikali ya kujenga mizani hizi nchini sio kutoza tozo bali ni kujenga utamaduni wa kutozidisha uzito ili kulinda barabara zetu", amesema Bashungwa.

Ameongeza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu ametoa fedha ya ujenzi wa njia nne wa barabara ya Nsalaga – Ifisi (km 29), ili kupunguza foleni katika barabara hiyo hivyo ni vema na mizani zitakazokuwepo ziendane na barabara hiyo.

Aidha, Bashungwa ametoa wito wa wasafirishaji wote nchini kuendelea kuzingatia viwango vya uzito vilivyotolewa kwa ajili ya kutumia barabara zetu ili kuendelea kuzilinda barabara na kuepuka kuingia gharama za tozo za kuzidisha uzito.

Naye, Mkurugenzi wa Miradi kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Eng. Boniface Mkumbo amesema mzani huo unasaidia kudhibiti magari ya mizigo na ya abiria yanaoenda /yanaotoka Malawi, Kyela na Rungwe.

Ameongeza kuwa katika Mkoa wa Mbeya kuna mizani miwili ambayo ni Uyole na Mbugani ambayo inatumika kwa udhibiti wa uzito wa magari.

"Mzani wa Uyole unapima mitarimbo kwa pamoja mitarimbo mitatu (Group Axle Weigher) wakati Mzani wa Mbugani (Chunya) unapima mtarimbo mmoja mmoja (Single Axle weigher)", amefafanua Eng. Mkumbo.



*Mkurugenzi wa Miradi kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Eng. Boniface Mkumbo, akitoa maelezo kwa Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, kuhusu Mzani wa kupima uzito wa magari wa Uyole uliopo mwanzoni mwa barabara ya Uyole - Kasumulu (mpakani mwa Tanzania na Malawi), mkoani Mbeya.*

**Mtandao wa Barabara unaosimamiwa na TANROADS una jumla ya mizani 76 ya Kudumu na inayofanya kazi ambapo kati ya hiyo mizani 58 haijawekwa mfumo wa kupima magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) na 15 imeshafungwa tayari ambayo ni Vigwaza North na Vigwaza South (Pwani), Mpemba (Songwe), Nala (Dodoma), Mikese South (Morogoro), Wenda North na Wenda South (Iringa), Njuki (Singida), Dakawa North na Dakawa South (Morogoro), Kimokouwa East na Kimokouwa West (Arusha).**




*Muonekano wa Mzani wa kupima uzito wa magari wa Uyole uliopo mwanzoni mwa barabara ya Uyole - Kasumulu (mpakani mwa Tanzania na Malawi), mkoani Mbeya.*




*Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, akifafanuliwa jambo na Msimamizi wa Mzani wa Uyole, Eng. Wawila Mwazembe. wakati akikagua mzani huo wa kupima uzito magari uliopo mwanzoni mwa barabara ya Uyole - Kasumulu (mpakani mwa Tanzania na Malawi), mkoani Mbeya.*



*Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, akizungumza na mmoja wa wasafirishaji wa mizigo wakati akikagua Mzani wa kupima uzito wa magari wa Uyole uliopo mwanzoni mwa barabara ya Uyole - Kasumulu (mpakani mwa Tanzania na Malawi), mkoani Mbeya.*

# DARAJA LA J.P MAGUFULI LIMEFIKIA 78%, MKANDARASI ANALIPWA KWA WAKATI

Na **Segolena Francis**



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa amesema kuwa serikali inalipa kwa wakati madai yote yanayowasilishwa na Mkandarasi anayetekeleza ujenzi wa daraja la J.P Magufuli (Kigongo – Busisi) lenye urefu wa kilomita 3.0 na Barabara unganishi zenye jumla ya kilometa 1.66 lililopo jijini Mwanza ambapo ujenzi umefikia asilimia 78 ya Utekelezaji.

Ameyasema hayo Oktoba 11, 2023 akiwa Mwanza katika ziara ya kukagua Daraja hilo linalounganisha Barabara Kuu ya Usagara - Sengerema - Geita katika Ziwa Victoria kwa kugharimiwa na Serikali kwa jumla ya shilingi Bilioni 716.3

Bashungwa amesema kuwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Ujenzi wa Daraja hilo ameupa kipaumbele kikubwa kwa kuhakikisha Mkandarasi hatoki nje ya mradi kwa kutoa fedha kuwezesha madai yote ya mkandarasi kulipwa ndani ya muda ili kuhakikisha anafanya kazi bila kusimama.

"Mheshimiwa Rais anaendelea kuonesha kwa vitendo kaulimbiu yake ya awamu ya sita ya kazi iendelee ambayo inamaanisha kijiti ambacho alikipokea kutoka kwa kaka yake Hayati Dkt. John Pombe Magufuli ameendeleza pale alipoishia ikiwemo mradi huu wa historia kwa nchi yetu" Amesema Bashungwa.

Aidha, Bashungwa ameeleza kuwa Mheshimiwa Rais anahakikisha hakuna madai yanayowasilishwa na mkandarasi huyo ambayo hayalipwi na amemuomba Mkuu wa Mkua wa Mwanza, Amos Makalla, kupita mara kwa mara katika mradi huo ili kuhakikisha kazi inaendelea kwa sababu mkandarasi hana sababu yeyote ya kutoendelea na kazi kwani malipo yote yanafanyika kwa wakati.

Amemshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuifungua Mikoa ya kanda ya ziwa ambapo kwa muunganiko wa Bandari pamoja na mradi wa Reli ya kisasa ya SGR, mizigo kutoka nchi mbali mbali duniani itatumia miundombinu hiyo kusafirisha mizigo yao na hivyo kunufaisha ukanda huu wa ziwa kwa kupitia kituo kikubwa cha SGR cha Misungwi.

"Tunaposema Kazi Iendelee ni kama hivi miradi yote inayotumia mabilioni ya fedha inatekelezwa hivyo nawaomba watanzania tuendelee kuwa wamoja kwani mradi huu utafungua fursa za kiuchumi kwa wananchi wa kanda ya ziwa na mikoa ya jirani" ameongeza Bashungwa.

Awali akitoa taarifa ya daraja hilo, Mkurugenzi wa Miradi kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Eng Boniface Mkumbo amesema kuwa hadi sasa mkandarasi ameshalipwa jumla ya shilingi bilioni 396.3 ambazo zinajumuisha malipo ya awali pamoja na hati zote za madai 17 alizowasilisha hivyo hadai malipo yoyote.

Amesema kuwa lengo la ujenzi wa daraja hilo ni kuunganisha barabara kuu ya Usagara – Kisesa – Geita yenye urefu wa kilomita 90 katika ushoroba wa ziwa Victoria ambayo inaanzia Sirari mpakani mwa Tanzania na Kenya hadi Mutukula mpakani mwa Tanzania na Uganda (km 774)

Mkumbo amesema kuwa kwa sasa barabara hii inaunganishwa kwa kutumia vivuko vikubwa vitatu na kutokana na idadi kubwa ya magari yanayopita kwa siku huweza kutumia masaa mawili hadi matatu kuvusha magari kutoka upande mmoja hadi mwingine.










# 'WATUMISHI TUNZENI SIRI ZA SERIKALI' LUDOVICK NDUHIYE

Na **Theresia Mwami**




*Naibu Katibu Mkuu Sekta ya Ujenzi, Ludovick Nduhiye akizungumza na Watumishi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara (RfB) (hawapo pichani) katika kikao kazi cha Wajumbe wa Menejimenti na watumishi wa bodi hiyo, Mkoani Singida.*

Watumishi wa Bodi ya Mfuko wa Barabara wametakiwa kuzingatia miiko na utunzaji siri za Serikali pamoja na kuongeza ari ya utendaji kazi na utekelezaji wa majukumu ya Bodi hiyo ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa kazi.

Akizungumza katika kikao cha Wajumbe wa Menejimenti na Watumishi wa Bodi ambacho kimefanyika mkoani Singida, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Ludovick nduhiye, amesema utoaji siri za Serikali ni jambo la hatari ambalo linaweza kusababisha taharuki kwa jamii.

Ameongeza kuwa, kikao hicho pia kitasaidia kubadilishana uzoefu, kujenga mshikamano na kuchochea morali ya kazi kwa watumishi hivyo kuongeza tija na ufanisi katika utendaji kazi wa bodi hiyo.

Baadhi ya Viongozi na Watumishi ambao wamehudhuria kikao hicho wameeleza umuhimu wa utunzaji siri na madhara ya kutofanya hivyo huku wakiwapongeza viongozi wa bodi hiyo kwa kuona haja ya kuwa na kikao kicho ambacho wanaamini kitakuwa mwarobaini wa kuondoa dosari zinazoweza kujitokeza katika utendaji kazi wa kila siku.

# UBORESHWAJI WA VIVUKO, SULUHU YA CHANGAMOTO ZA USAFIRI KWA WANANCHI

Na **Shukuru Senkondo**




*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA), Lazaro Kihalahala kushoto akisaini mkataba wa ujenzi wa kivuko kipya cha Buyagu Mbalika na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Songoro Major Songoro kulia katika hafla fupi ya utiaji saini iliyofanyika viwanja vya Sabasaba Wilayani Sengerema Mkoani Mwanza.*

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, inafanya jitihada mbalimbali kuhakikisha huduma za usafiri na usafirishaji zinaimarika katika maeneo mbalimbali nchini.

Maeneo hayo ni pamoja na anga , nchi kavu pamoja na majini na huku uimarishaji wake ukijikita katika ununuzi na ujenzi wa vifaa vipya na vya kisasa lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma za uhakika.

Mathalani, kwa upande wa usafiri wa majini hususan Vivuko, serikali imekuwa ikinunua na kujenga vivuko katika maeneo mbalimbali ikiwemo ya kanda ya Ziwa ambapo usafiri huu umeonekana kuwa ni mkombozi kwa wananchi wa maeneo hayo.

Kwa kuzingatia hilo , hivi karibuni tumeshuhudia utiaji saini wa mikataba mikubwa ya ujenzi wa vivuko ikiwamo ujenzi wa kivuko kipya cha Buyagu Mbalika jijini Mwanza chenye thamani ya bilioni 3.8, mkataba huo uliosainiwa tarehe 23 Aprili 2023 na kushudiwa na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi ) Mhe. Godfrey Kasekenya huku Mkandarasi akiwa ni Kampuni ya Kizalendo ya Songoro Marine Transport Limited.

Akiwa katika hafla hiyo, Naibu Waziri Kasekenya alitaja faida za ujenzi wa kivuko hicho kwa kusema kuwa ujenzi utakapokamilika utaharakisha shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa wananchi waishio katika Wilaya ya Sengerema, Misungwi na maeneo mengine, aidha inatarajiwa kuwa na usafiri wa uhakika wenye huduma bora na salama katika maeneo ya Buyagu na Mbalika.

Naye Mtendaji Mkuu wa Wakala huo Lazaro Kilahala amesema hitaji la kivuko cha uhakika baina ya Buyagu na Mbalika limekuwa ni kilio



cha muda mrefu kwa wananchi wa maeneo hayo hivyo ujenzi wa kivuko hicho utakapokamilika utaondoa kero nyingi za kiuchumi na kijamii ambazo zimekuwa zikichelewesha maendeleo ya wananchi hao hivyo kutimiza azma ya Serikali kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Kilahala ameeleza kuwa katika mwaka huu wa fedha, Wakala unaendelea na ujenzi wa vivuko vipya vitano vyenye thamani jumla ya Bilioni 33.2 vitakavyotoa huduma kwenye vituo vya Kisorya - Rugezi, Bwiro – Bukondo, Nyakarilo – Kome, Ijinga – Kahangala na Mafia – Nyamisati hivyo kivuko cha Buyagu-Mbalika ambacho leo mkataba wake wa Ujenzi umesainiwa ni kivuko cha sita (6) ambacho Ujenzi wake unaanza katika mwaka huu wa fedha.

Aliongeza kuwa sambamba na Ujenzi wa vivuko vipya katika mwaka wa fedha 2022/23 Serikali kupitia Wakala inafanya ukarabati wa vivuko 18 pamoja na Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vivuko katika maeneo 11 ya huduma kwa gharama ya bilioni 27.5.

Halikadhalika, mapema mwaka huu Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhe. Mhandisi Godfrey Kasekenya alipata wasaa wa kukagua karakana ya ujenzi wa meli na vivuko ya Songoro jijini Mwanza na kupata taarifa ya maendeleo ya ujenzi na ukarabati wa vivuko hivyo vitakavyogharimu takribani bilioni 26 na kutarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Agosti mwaka huu.

Aidha, Imeelezwa kuwa kukamilika kwa ujenzi wa vivuko vipya vinne na ukarabati wa vivuko vinne vitakavyotoa huduma katika maeneo mbalimbali ya Ziwa Victoria kutapunguza changamoto za usafiri kwa wananchi wanaoishi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na kutarahisisha shughuli za maisha kwa urahisi, uhakika na usalama.

Naye, Kaimu Meneja Vivuko Kanda ya Ziwa na Magharibi kutoka TEMESA Mhandisi, Aloyce Ndunguru, alisema kuwa wanaendelea na ujenzi wa vituo vipya vitatu ambavyo ni Bwiro (kisiwani) – Bukondo katika Wilaya ya Ukerewe, Kituo cha Ijinga (kisiwani) – Kahangala katika Wilaya ya Magu na Kituo cha Mayenzi – Kanyinya ambapo miradi hiyo ikikamilika itafanya wawe na jumla ya vituo 16 katika kanda hiyo.

Alieleza pia kanda hiyo ina jumla ya vivuko 17 ambapo kati ya hivyo vivuko vinne vipo katika matengenezo makubwa ambavyo ni MV Misungwi (Kigongo - Busisi), MV Mara (Iramba - Majita), MV Ujenzi (Kisorya - Rugezi) na MV Nyerere (Bugolora - Ukara).

Katika bajeti ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 mradi wa ujenzi na ukarabati wa vivuko na maegesho ya vivuko, umetengewa jumla ya shilingi bilioni 14.3 ambapo mradi wa ujenzi wa vivuko vipya umetengewa bilioni 5.7 kwa ajili ya ununuzi wa vivuko vipya vya Kisorya-Rugezi, Ijinga - Kahalanga, Bwiro-Bukondo, Nyakarilo - Kome, Nyamisati - Mafia na Buyagu - Mbalika.

Kazi nyingine ni ununuzi wa boti mbili ndogo (Sea taxi ferries) zitakazotoa huduma katika kituo cha Magogoni-Kigamboni , ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA, huduma za ushauri pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa miradi hiyo.

Pia mradi wa kukarabati wa vivuko umetengewa jumla ya bilioni 6,089 kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa kivuko Mv Ujenzi, Mv Mara,Mv Kome II, Mv Malagarasi, Mv Mafanikio, Mv Misungwi , Mv Nyerere,Mv Kyanyabasa, Mv Tanga na Mv Kitunda.

Aidha kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa vivuko Mv Mwanza, Mv Kigamboni, Mv Ukara 1, Mv Ukara II, Mv sabasaba , Mv Pangani II na ukarabati wa boti ya uokozi ya Mv SAR II , ukarabati wa kivuko Mv Kilombero II na kukihamisha kwenda Mlimba- Malinyi pamoja na ufuatiliaji wa tathmini ya miradi hiyo.

Ni dhahiri kuwa Serikali imejizatiti vya kutosha kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora za usafiri na usafirishaji zinazochochea ukuaji wa uchumi, ni wajibu wetu sisi kama wananchi kuhakikisha tunatunza vyema rasilimali zetu na kuzilinda kwa faida ya sasa na vizazi vijavyo.

# BASHUNGWA AJA NA MUAROBAINI WADAIWA SUGU TBA

Na **Segolena Francis**



*Waziri wa Ujenzi, Mhe. Innocent L. Bashungwa (Mb) akizungumza na Menejimenti ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) wakati wa ziara yake ya kwanza katika taasisi tangu alipoteuliwa kuwa Waziri wa Ujenzi, tarehe 07 Septemba 2023 jijini Dodoma.*

Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, ameuagiza Wakala wa Majengo (TBA), kuhakikisha unakusanya deni la Shilingi Bilioni 81.5 wanazodai kwa wapangaji wao sambamba na kuwaondoa wadaiwa sugu katika nyumba hizo ili upatikanaji wa fedha hizo uweze kusaidia utekelezaji wa miradi mingine nchini.

"TBA simamieni sheria kwa yeyote asiyelipa kodi hata kama ni kiongozi, waandikieni notisi ya kulipa madeni yao na wasipolipa waondoeeni, wapo wengine nje wanasubiri wapewe nyumba ili waweze kulipa kodi kwa wakati na tutamia makusanya hayo kujenga nyumba nyingine", amesisitiza Bashungwa.

Ameyasema hayo leo Septemba 07, 2023 jijini Dodoma wakati Waziri huyo alipofanya ziara yake kwa mara ya kwanza katika Wakala huo na kuzungumza na menejimenti ya TBA ambapo amesisitiza uwekezaji wenye tija kwa watumishi na Taifa kwa ujumla.

Aidha, Bashungwa ameagiza TBA kuhakikisha wanakuja na mikakati itakayosaidia kujenga nyumba za bei nafuu hasa kwa vijana wanaoajiriwa katika utumishi wa umma hususan Dodoma ili kuweza kumudu gharama za maisha.

"Kuna vijana ambao wanaingia kwenye kada ya utumishi wa umma na bado hawajawa na uwezo wa kujijengea nyumba, kupitia TBA mnaweza kujenga nyumba za bei rahisi kwa ajili ya vijana hao ili kuwarahisishia gharama za Maisha", amesema Bashungwa.

Kadhalika, Bashungwa ameutaka Wakala huo kuwa na utaratibu wa kuwajengea uwezo wataalamu walionao ili kuenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya teknolojia hasa

katika suala la ujenzi na uendelezaji wa majengo mbalimbali.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa TBA, Arch. Daud Kondoro, amesema kuwa Wakala huo utahakikisha unatafuta ufumbuzi wa changamoto zilizopo na kumuahidi Waziri Bashungwa kuandaa mikakati mizuri itakayosaidia Wakala huo kutoa huduma bora kwa wananchi.

Awali wakati akitoa taarifa yake kwa Waziri huyo, Arch. Kondoro ameeleza kuwa hadi sasa TBA inaendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 3500 za watumishi wa umma eneo la Nzuguni Dodoma ambapo awamu ya kwanza ya nyumba 150 utekelezaji umefikia asilimia 95 na awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 150 utekelezaji wake umefikia asilimia 10.

Miradi mingine ni ujenzi wa nyumba 20 za Viongozi jijini Dodoma ambazo zililenga kukabiliana na uhaba wa nyumba za Viongozi baada ya Serikali kuhamia Dodoma ambapo mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 na nyumba zimeanza kutumiwa na Viongozi.







*Waziri wa Ujenzi, Mhe. Innocent L. Bashungwa (Katikati) akizungumza na Menejimenti ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) wakati wa ziara yake katika taasisi hiyo, tarehe 07 Septemba 2023 jijini Dodoma. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Balozi Mhandisi Aisha Amour, kulia Mtendaji Mkuu wa TBA, Arch. Daud Kondoro.*

# MIUNDOMBINU YA BARABARA KUIFUNGUA MIKOA YA KUSINI KIUCHUMI

Na **Siti Said**




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt.Samia Suluhu Hassan akiweka jiwe la msingi la ufunguzi wa barabara ya Mtwara-Newala-Masasi, sehemu ya Mtwara-Mnivata (Km 50) iliyogharamiwa na Serikali kwa asilimia 100 kwa gharama ya shilingi Bilioni 93.83 leo tarehe 15 Septemba 2023. Kushoto ni Waziri wa Ujenzi Mhe. Innocent Bashungwa.*

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kuhakikisha inajenga na kuboresha miundombinu ya barabara nchini, lengo ni kumrahisishia mwananchi huduma za usafiri na usafirishaji.

Halikadhalika Serikali imekuwa ikijenga miundombinu ya barabara katika maeneo mbalimbali nchini kwa kutumia fedha za wahisani kama Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na wahisani wengine mbalimbali pamoja na kutumia fedha zake za ndani. Pia Serikali inahakikisha miundombinu hii inajengwa mijini na vijijini ili kila mwananchi afikiwe na huduma hii muhimu ambayo ni uti wa mgongo katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Watafiti wa masuala ya kiuchumi huamini kwamba miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwa imara, hata uchumi katika eneo husika utakuwa imara kutokana na kuwa sehemu ambayo miundombinu inapita kama barabara, reli na viwanja vya ndege, shughuli mbalimbali za kimaendeleo hufanyika ikiwemo kilimo, utalii, biashara na hata uwekezaji wa viwanda.

Kwa mantiki hii, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan, amehakikisha anajenga na kuboresha miundombinu hii nchini ambapo hivi karibuni Rais Dkt. Samia aliweka mawe ya msingi ya Ujenzi na Ufunguzi wa barabara katika mikoa ya Mtwara na Lindi wakati alipofanya ziara yake katika mikoa hiyo ambayo ni maarufu sana kwa ulimaji wa korosho, ufuta na mbaazi.

Akiwa katika mikoa hiyo, Rais Samia aliweka Mawe ya Msingi katika Ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Nachingwea – Ruangwa - Nanganga, sehemu ya Ruangwa

– Nanganga (km 53.2) na barabara ya Mtwara - Newala - Masasi (km 210); sehemu ya Mnivata - Newala - Masasi (km 160) pamoja na kufungua barabara ya Mtwara- Newala-Masasi, sehemu ya Mtwara-Mnivata (Km 50) iliyogharamiwa na Serikali kwa asilimia 100 kwa gharama ya shilingi Bilioni 93.83.

Wakati akizindua ujenzi wa barabara hizo, Rais Dkt. Samia alisema Serikali ya awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejipanga kujenga miundombinu ya mikoa ya kusini ili kurahisisha usafirshaji wa mazao na kukuza uchumi wa mikoa hiyo na kuwataka wakandarasi wakamilishe ujenzi wa barabara hizo kwa wakati.

“Niwaombe wakandarasi na wasimamizi waende kwa kasi sana lakini nipongeze TANROADS, mkandarasi na wengine kwa hatua ambayo imeshafikia, na kwetu sisi Serikali mafedha yapo tunasubiri certificate (cheti) ziletwe tulipe, halafu kazi ziendelee”- alisema Rais Dkt. Samia.

Rais Samia alisema lengo la Serikali ni kuunganisha mikoa yote ya Mtwara na Lindi pamoja na wilaya zake kwa kiwango cha lami.

“Niwaombe mpokee maendeleo yanayokuja tufanye kazi kwa pamoja, langu kubwa la kuwaomba ni maendeleo, na maendeleo ni fedha ndugu zangu na fedha inapatikana tunapouza bidhaa na nyinyi ni wakulima wazuri wa ufuta, mbaazi na koroshop na bei ya ufuta na mbaazi mmeiona mwaka huu, tunafanya kazi tuone korosho nayo iwe na bei nzuri”- alisisitiza Rais Samia

Kwa upande wake, Waziri wa Ujenzi, Mhe. Innocent L. Bashungwa alisema shilingi Bilioni 268 zimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi wa ujenzi wa barabara ya Mtwara - Newala Masasi (km 210); sehemu ya



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, Waziri wa Ujenzi, Mhe. Innocent Bashungwa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhe. Mohamed Mchengerwa na viongozi wengine akiweka Jiwe la Msingi la Ujenzi wa Barabara ya Nachingwea – Ruangwa, sehemu ya Ruangwa – Nanganga (km 53.2) inayojengwa kwa kiwango cha lami, leo tarehe 18 Septemba 2023.*




*Muonekano wa Barabara ya Mtwara - Newala- Masasi, sehemu ya Mtwara - Mnivata (Km 50) ambayo imefunguliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan leo tarehe 15 Septemba 2023.*

Mnivata - Newala - Masasi (km 160) kwa kiwango cha lami ili kuufungua mkoa wa Mtwara kiuchumi, kijamii na kuchochea biashara katika ukanda huo wa Mikoa ya Kusini.

Alifafanua kuwa ukamilishaji wa mradi huo kwa ujumla utagharimu kiasi cha shilingi Bilioni 361 na miradi hiyo itatekelezwa kwa muda wa miezi 36.

Waziri Bashungwa alieleza hayo wakati akizungumza katika mkutano wa hadhara wa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliofanyika katika uwanja wa Nangwanda Sijaona , Septemba 15, 2023.

Waziri Bashungwa alieleza kuwa mpaka sasa Sehemu ya barabara ya Mnivata – Mitesa (km 100), Mkandarasi amekwishakabidhiwa eneo la mradi kwa ajili ya kuanza utekelezaji na Sehemu ya Mitesa – Masasi (km 60) pamoja na Ujenzi wa Daraja la Mwiti taratibu za kumpata mkandarasi ziko katika hatua za mwisho.

Alisema shilingi bilioni 400 zitatumika katika ukarabati wa Barabara ya Mtwara-Mingoyo-Masasi kupitia majadiliano yaliyofanywa kati ya Serikali na Benki ya Dunia (WB).
Pia, alimpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi wa barabara inayounganisha vipande kutoka Masasi- Nachingwea - Liwale (km 175).

Kuhusu Barabara ya Nangurukuru - Liwale (km 230) Waziri Bashungwa alisema tayari Serikali imetenga fedha za kuanza ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 72 kuanzia Liwale hadi Choya.

"Mhe. Rais kama hiyo haitoshi kipo kipande cha Barabara ya Ruangwa-Namichiga kilometa 20 ambacho kwa sasa kipo kwenye mipango ya kuwekwa lami kupitia mradi wa RISE, sasa ukiona mahaba na Watanzania wakijitokeza kwa wingi unakopita ni kwamba wewe ni Rais wa vitendo na wanaona kazi kubwa ya Serikali unayoiongoza", alisema Bashungwa.

Aidha, alileza kuwa Wizara inaendelea na juhudi za kuunganisha sehemu mbalimbali za mikoa ya nchi yetu na nchi jirani kwa barabara za lami zikiwemo nchi za Msumbiji, Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya.

"Baadhi ya barabara zilizokwishakamilishwa kwa kiwango cha lami na kuunganisha nchi yetu na nchi jirani ni Mtwara – Lindi (Mingoyo) – Masasi – Tunduru – Ruvuma hadi Mbambabay; Songea – Makambako; na barabara ya TANZAM highway", amefafanua Waziri Bashungwa.

Alitaja miradi mingine ya barabara inayoendelea mkoani humo ikiwemo barabara ya Masasi – Nachingwea – Liwale (km 175) kwa Kiwango cha Lami kwa utaratibu wa Uhandisi, Ununuzi, Ujenzi na Fedha (EPC+F) ambao mkataba wake ulisainiwa Juni 16, 2023 kati ya TANROADS na Mkandarasi M/S China Railway 15 Bureau Group Co. Ltd.

Kadhalika, Waziri Bashungwa alimhakikishia Rais Dkt. Samia kuwa Wizara itahakikisha Taasisi za Kikandarasi na Kihandisi zilizo chini yake, zinatumika vizuri katika kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi nchini, na kuhakikisha kazi zinakamilika kwa viwango vinavyokubalika kimikataba, kwa muda uliopangwa, ili Wananchi wapate huduma iliyokusudiwa kwa wakati.

Kuhusu uwekaji wa taa za barabarani, Waziri Bashungwa alisema kuwa Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara (TANROADS) itahakikisha inatenga bajeti ya kutosha ya kuweka taa katika barabara zote zinazopita katika miji ili kuimarisha ulinzi na usalama kwa wananchi katika maeneo hayo.

"Serikali imetenga Shilingi Bilioni 1.3 kuweka taa za barabarani katika maeneo ya Mangaka, Masasi na Nanyumbu ambapo taa hizo zinawekwa hivi karibuni kwani fedha yake ipo", alisema Bashungwa.

Akisoma taarifa fupi ya ujenzi wa barabara ya Nachingwea – Ruangwa - Nanganga, sehemu ya Ruangwa – Nanganga (km 53.2) inayojengwa kwa kiwango cha lami, mbele ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mhandisi Mohamed Besta, alisema mkandarasi anayejenga barabara hiyo ni China 15th Group kwa thamani ya Shilingi Bilioni 50.3 na jumla ya Shilingi Bilioni 1.1 ikiwa ni sehemu ya Ongezeko la thamani na kutumika kulipa fidia ya mali na ardhi kwa watu walioathirika na ujenzi kwa mujibu wa Sheria.

*Bil. 268 kukamilisha Barabara ya Mnivata-Newala-Masasi (Km 160) kwa kiwango cha lami*

*Bil 1.3 kuweka Taa za barabarani kuimarisha ulinzi na usalama*

*Miradi mingine ya barabara kujengwa mkoani Mtwara na Lindi*

"Mheshimiwa Rais ujenzi wa Barabara unasimamiwa na TEKU ambacho ni kitengo cha TANROADS na maendeleo ya ujenzi mpaka sasa tumefikia asilimia 71, na mapaka sasa tumeshalipa jumla ya shilingi Bilioni 20.7 na zilizobaki tunaendelea kulipa kwa utaratibu uliowekwa", alisema Mhandisi Besta.

Kwa ujumla Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan "bado yupo kazini", hii inamaanisha kuwa anahakikisha mikoa yote pamoja na wilaya zake zilizopo nchi nzima inaunganishwa na barabara za lami na anahakikisha kuwa miradi mingine ya kimaendeleo ikiwemo ujenzi wa viwanja vya ndege, reli na miundombinu mengine inaendelea ili kurahisisha huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia zote zinakuwa bora na za uhakika kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

# MAKANDARASI WAZAWA WAFUNDWA KIBIASHARA

Na **Neema Macha**



*Msajili wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Mhandisi Rhoben Nkori (wanne kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na makandarasi mara baada ya kufungua mafunzo ya kibiashara kwa makandarasi hao, yaliyofanyika jijini Dodoma.*

Makandarasi wazawa wametakiwa kuzisimamia kampuni zao kwa ufasaha kwa kufuata sheria za ulipaji wa kodi kwa wakati na kufanya kazi kwa weledi kwa kutumia wataalamu stahiki katika sekta mbalimbali ili kukwepa changamoto katika maeneo yao ya kazi.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo yenye lengo la kuwajengea uwezo Makandarasi wazawa kibiashara, jijini Dodoma, Msajili wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Mha. Rhobin Nkori, alisema kuwa lengo moja wapo la kufanya mafunzo hayo ni pamoja na kutoa elimu kwa makandarasi kuhusiana na mvutano baina yao na mamlaka ya mapato Tanzania (TRA).

“Nimefurahi kuona kwamba moja ya mada itakayofundishwa ni kuhusu masuala ya kodi kwa makandarasi, hii itatusaidia kupunguza matatizo makubwa sana kati ya wakandarasi na TRA”, alisema Msajili.

Aidha Mha. Nkori, alisema makampuni mengine hutumika kufanya kazi kwa majina ya wamiliki wengine yanayopelekea mvutano pindi kazi inapoenda kukaguliwa na TRA kupitia Bodi ya Usajili wa Makandarasi(CRB) hivyo amewataka wamiliki wa makampuni kusimamia vyema makampuni yao ili kuepuka changamoto hizo.

Mha. Nkori amesisitiza kuwa ili kuendelea kujenga taswira nzuri kwa makandarasi nchini, Bodi itaendelea kuwachukulia hatua kisheria makandarasi wote wanaokiuka maadili yao ya kazi.

Naye, Mkurugenzi wa kampuni ya SONCO ENGINEERING COMPANY LIMITED, Mha. Baraka Materu, ameiomba serikali kuweka mikakati maalumu ya kuwashirikisha wakandarasi wazawa wakati wa utekelezaji wa miradi mikubwa ili kuwajengea uwezo makandarasi hao kutokana na teknolojia mpya ambayo watajifunza kupitia miradi hiyo.

Mafunzo hayo ya siku tatu yaliyotolewa na Bodi hiyo yameshirikisha makandarasi kutoka sehemu mbalimbali nchini lengo likiwa ni kubadilishana uzoefu na kuwajengea uwezo makandarasi hao katika mujukumu yao ya kazi.

# BASHUNGWA AMVAA MKANDARASI BARABARA YA MZUNGUKO WA NJE YA DODOMA

Na **Siti Said**



*Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, akitoa maelekezo kwa mkandarasi wa Kampuni ya Avic wakati alipokagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje ya Dodoma yenye jumla ya urefu wa kilometa 112.3; sehemu ya Ihumwa Dry Port - Matumbulu - Nala (km 60), Septemba 29, 2023 jijini Dodoma.*

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa amemuagiza Mkandarasi Avic anayejenga barabara ya mzunguko wa nje ya Dodoma, yenye urefu wa Kilometa 112.3 sehemu ya Ihumwa Dry Port - Matumbulu - Nala (km 60), kuhakikisha anakamilisha barabara hiyo ifikapo mwezi Desemba, 2024.

Bashungwa ametoa agizo hilo Septemba 29, 2023, jijini Dodoma wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo ambapo pamoja na mambo mengine amemsisitiza mkandarasi huyo kuongeza spidi kwenye ujenzi wa madaraja mawili ambayo yanaonekana kuchelewa ujenzi wake.

"Sipepesi macho kwenye usimamizi wa mikataba, kufanya kazi kwa ubora na kasi ndio kipimo chako, ukizembea kwenye kazi hii usahau kupewa kazi nyingine za ujenzi kwenye Sekta hii nchini", amesema Bashungwa.

Ameahidi kutembelea tena mradi huo ifikapo Desemba mwaka huu ili kuona uetekelezaji wa maagizo yake na kumsisitiza Mkandarasi huyo kufanya kazi usiku na mchana ili uweze kukamilika kwa wakati kulingana na maelekezo ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Aidha, Bashungwa ameuagiza Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS), kushirikiana na Shirika la Reli (TRC), kurudisha haraka mawasiliano ya barabara ya lami eneo la Mkonze na Nala ambalo lilibomolewa kwa ajili ya ujenzi wa reli ya SGR kwani wananchi wamekuwa wakipata kero kutokana na changamoto katika maeneo hayo.

Bashungwa amewataka wakandarasi nchini wanaotekeleza miradi ya ujenzi kuhakikisha wanatekeleza miradi hiyo kwa mujibu wa Mkataba na kusisitiza kutokuwa na huruma kwa yeyote atakayekiuka mikataba hiyo.

Bashungwa amemuagiza Mhandisi Mshauri Mzawa wa kampuni ya Inter-Consult kumsimamia mkandarasi wa kampuni ya China Civil Engineering Corporation (CCEC) anayetekeleza sehemu ya Nala - Veyula - Mtumba (km 52.3), kutoa vifaa vya usalama kwa wafanyakazi wake ili kuepukana na madhara yanayoweza kutokea maeneo ya kazi.

Katika hatua nyingine, Bashungwa amewaagiza Mameneja wa TANROADS wa mikoa yote nchini kuhakikisha wanazibua mifereji ya barabara zilizo chini ya Wakala huo kabla ya mvua hazijaanza ili zisiwe chanzo cha kuleta mafuriko, sambamba na hilo Waziri huyo amempongeza Meneja wa TANRODS Mkoa wa Dar es Salaam kwa kufanya matengenezo na kuzibua barabara na mifereji katika mkoa huo.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Eng. Mohamed Besta ameeleza kuwa mpaka sasa sehemu ya mradi kutoka Nala – Veyula – Mtumba (km 52.3) umefika asilimia 54.3 na sehemu inayoanzia Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala umefika asilimia 50 na sasa wakandarasi wanaendelea na kazi mbalimbali za ujenzi wa makalavati na madaraja makubwa mawili.







*Muonekano wa sehemu ya barabara ya mzunguko wa nje ya Dodoma (km 112.3) inayojengwa kwa kiwango cha lami. Ujenzi wake unagharimiwa na Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa gharama ya shilingi Bilioni 221.*

# KASEKENYA AZITAKA TEMESA NA TANROADS DODOMA KUJIPANGA KIMKAKATI

Na **Shukuru Senkondo**



*Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, akikagua mashine ya kupima ubora wa vifaa vya ujenzi, alipokagua maabara ya vifaa vya wakala huo jijini Dodoma.*

Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya amezitaka Taasisi za Wakala wa Barabara (TANROADS) na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) mkoani Dodoma kuweka mikakati ya kufanya kazi kitaifa badala ya kufanya kazi kimkoa kama ilivyokuwa awali.

Akizungumza alipokagua karakana ya TEMESA Mkoa wa Dodoma na maabara ya kupima vifaa vya ujenzi ya TANROADS, mkoani humo Naibu Waziri Kasekenya, amehimiza kuwa ni vyema taasisi hizo zikajiimarisha kuhudumia watu wengi waliohamia katika makoa makuu ya nchi kwa kuboresa idadi ya wataalamu, vifaa na kufanya kazi zenye ubora kwa muda mfupi.

“TEMESA himizeni ubunifu na uadilifu kwa watumishi wenu ili Taasisi nyingi na watu binafsi wavutiwe kutengeneza magari yao katika karakana yenu na kunufaika na utaalamu wa huduma nyingine za masuala ya umeme mnazotoa”, amesema Naibu Waziri Kasekenya.

Amezungumzia umuhimu wa TEMESA kuwaelimisha wateja wao umuhimu wa kuondoa magari mabovu yaliyotelekezwa katika karakana hizo ili kupata nafasi ya kutosha kuhudumia idadi kubwa ya magari inayohudumiwa na karakana hiyo.

Aidha, amezitaka TEMESA na TANROADS kuendelea kutoa fursa kwa wanafunzi wenye taaluma ya uhandisi kufanya mazoezi ya vitendo ili kuwajengea uwezo vijana wengi zaidi na kuwafundisha ubunifu.




*Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, akizungumza na mafundi wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Mkoa wa Dodoma alipokagua maendeleo ya karakana ya Wakala huo.*



*Meneja wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) Mkoa wa Dodoma, Eng. Grayson Maleko (kulia), akifafanua jambo kwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya (katikati).*



*Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, akitoa maelekezo kwa Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Dodoma Eng. Leonard Chimagu.*



*Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, akisisitiza jambo kwa Meneja wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Mkoa wa Dodoma, Eng. Grayson Maleko (kulia).*

Kwa upande wake, Meneja wa TEMESA mkoa wa Dodoma, Eng. Grayson Maleko, amemuomba Naibu Waziri huyo kusaidia Taasisi hiyo kupata watumishi wa kutosha ili kuongeza tija na kuwezesha kufikia malengo waliyojiwekea.

Naye, Meneja wa TANROADS mkoa wa Dodoma, Eng. Leonard Chimagu, amemhakikishia Naibu Waziri kuwa TANROADS imejipanga kuhakikisha miradi yote ya ujenzi inayoendelea jijini Dodoma inasimamiwa kikamilifu na kukamilka kwa wakati.

Naibu Waziri Kasekenya, alikuwa katika ziara ya kukagua utendaji wa TEMESA na TANROADS ili kujionea namna taasisi hizo zinavyoendana na mabadiliko na kuhudumia idadi kubwa ya watu kwa kuwa katika makao makuu ya nchi.



*Naibu Waziri wa Ujenzi, Eng. Godfrey Kasekenya, akitoa maelekezo kwa Meneja wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Mkoa wa Dodoma, Eng. Grayson Maleko (kulia), kuhusu kuhamisha magari chakavu yaliyotelekezwa, alipokagua maendeleo ya karakana ya Wakala huo Jijini Dodoma.*

# UKAGUZI UJENZI WA BARABARA YA LAMI YA BUGENE – BENACO

Na **Segolena Francis**



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa amesema kuwa Serikali itahakikisha inamlipa kwa wakati Mkandarasi M/s China Road and Bridge Cooperation anayejenga barabara ya Bugene – Kasulo (Beneco) – Kamunazi (km 128.5) kwa kiwango cha lami sehemu ya Bugene – Burigi Chato yenye urefu wa kilometa 60.

Amesema hayo Oktoba 12, 2023 wakati akizungumza na wananchi wa kata ya Nyaishozi mara baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi huo na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kulipa kwa wakati madai mengine yatakayowasilishwa na mkandarasi huyo ili aweze kuongeza kasi ya ujenzi pamoja na kulipa fidia kiasi cha bilioni 2 kwa wananchi waliopisha ujenzi wa barabara hiyo.

"Kuhusu fidia naomba niwaambie, mtupe kama mwezi mmoja kuanzia hii leo, tutakuwa tumekamilisha na hizo bilioni 2.074 zitakuwa zimeshakuja ndani ya wilaya ya Karagwe na wale ambao mmesubiri kwa muda mrefu tunaenda kuweka historia" amesema Bashungwa.

Bashungwa amewataka wananchi wa kata ya Nyaishozi kujipanga na kuhakikisha wanaweka mipango miji vizuri kwani Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaleta maendeleo kupitia miundombinu ikiwemo ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kwenda nchi za jirani.

Aidha, Bashungwa wakati akikagua eneo la mlima kihanga, kuangalia changamato zinazowapata watumiaji wa vyombo vya moto katika mlima huo na kuahidi kuwa wizara itafanya haraka kutatua changamoto katika eneo hilo.

Ametoa wito kwa Madereva wanaoendesha vyombo vya moto kuheshimu tahadhari na onyo ambazo zinatolewa kwenye vibao ambavyo vimewekwa barabarani kwani vimewekwa ili kulinda na kusaidia

usalama barabarani.

“Umahiri wa dereva sio kukimbia sana kutoka sehemu moja kwenda nyingine, bali ni kuhakikisha abiria waliopo kwenye chomba chake wapo salama, hivyo pamoja na marekebisho ambayo sio suluhisho kwa asilimia 100 bado madereva wanatakiwa kuhakikisha wanazingatia masuala ya usalama barabarani ikiwemo kuacha tabia ya mwendo kasi “, ameongeza Bashungwa.

Awali akitoa taarifa ya kukabiliana na tatizo la ajali eneo mlima Kihanga, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) Kagera Eng. Ntuli Mwaikokesya amesema kuwa wamejipanga kuongeza alama za tahadhari pamoja na kuweka taa sita kwenye eneo hilo ili alama hizo ziweze kuonekana nyakati za usiku hususani kwa madereva wageni ambao hupata ajali mara kwa mara.

Kuhusu barabara ya Bugene - Burigi Chato Eng. Mwaikokesya amesema kuwa ujenzi huo umefikia asilimia 27.7 na kwamba mara baada ya malipo hayo kufanyika Mkandarasi ataongeza timu za ujenzi wa barabara na makalvati pamoja na kufanya kazi usiku na mchana ili kufidia muda uliopotea.

Ukaguzi wa miradi inayoendelea ni muendelezo wa ziara ya Waziri Bashungwa kukagua miradi inayotekelezwa na Wizara yake katika mikoa mbalimbali nchini aliyoanzia mkoani Mbeya, Iringa, Singida, Simiyu, Mara, Mwanza na Kagera kuona maendeleo ya miradi hiyo na hatua za utekelezaji wake sambamba na ubora wa kazi zinazoendelea katika miradi hiyo.







# BASHUNGWA AKERWA NA KASI YA UJENZI MSALATO AIRPORT

Na **Deniza Cyprian**




*Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, akitoa maelekezo kwa mkandarasi wa Kampuni ya Beijing Construction Engineering Group wakati alipokagua maendeleo ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, Septemba 29, 2023 jijini Dodoma.*

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, ameagiza kampuni ya Beijing Construction Engineering Group kuhakikisha inakamilisha ujenzi wa jengo la abiria na jengo la kuogozea ndege katika Kiwanja cha Kimataifa cha Msalato, Dodoma ifikapo Desemba, 2024 kulingana na maelekezo ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Bashungwa amesema hayo leo Septemba 28, 2023 jijini Dodoma wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa kiwanja hicho na kutokuridhishwa na kasi ya maendeleo yake kutokana na kusuasua kwa mkandarasi huyo. “Mkandarasi usivimbe kichwa kana kwamba umepata kazi nyingi, usipozingatia maelekezo ambayo nimekupatia, kulingana na vipengele vilivyopo kwenye mkataba, tunaweza kukusimamisha kazi kwa mujibu wa sheria “ amesema Bashungwa.

Amemtahadharisha Mkandarasi huyo iwapo atazembea kukamilisha kazi hiyo kwa wakati itampelekea kutopata kazi nyingine katika Sekta ya Ujenzi ndani ya nchi. “Ukizembea kwenye kazi hizi, nina mamalaka ya kuhakikisha hupati kazi nyingine ndani ya nchi hii, baada ya ziara hii nataka kuona kazi inaenda kwa spidi”, amesisitiza Bashungwa.

Aidha, Bashungwa amemtaka Meneja Mkazi wa Kampuni hiyo kuripoti ofisini kwake na kumuandikia maelezo ya mpango kazi wake na ‘commitment letter’ ya kukamilisha mradi huo kwa wakati. Ameelekeza msimamizi wa miradi kutoka Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) kahakikisha anasimamia mradi huo masaa 24 ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa ubora na kwa wakati kama ilivyopangwa.

Bashungwa amebainisha kuwa ujenzi wa jengo hilo unatekelezwa kwa awamu mbili ambapo sehemu ya kwanza inahusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua kwa ndege yenye urefu km 3.6, maegesho ya ndege, Tax way, barabara za maingilio ambapo hadi sasa utekelezaji wake ni asilimia 36 huku, sehemu ya pili inahusisha ujenzi wa jengo la abiria pamoja na jengo la kuongozea ndege na miundombinu mengine ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 7.

Awali wakati akikagua barababara ya kuruka na kutua ndege, Bashungwa amempongeza mkandarasi Sinohydro Corporation anayeshirikiana na M/s Beijing Sino – Aero Construction Engineering na M/s China Jiangxi International Economic and Technical Cooperation kwa kuendelea kutekeleza mradi huo na kumsisitiza kuendelea kufanya kazi usiku na mchana ili uweze kumalizika kwa wakati.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Eng. Mohamed Besta amesema kuwa watahakikisha wanawasimamia wakandarasi wote wawili wanaojenga Kiwanja hicho ili kumalizika ndani ya muda kwa kuweka sawa ratiba yao ili iendane na muda waliopangiwa na kupata matokeo yanayoyatarajia.

Ukamilikaji wa kiwanja hicho ambacho sehemu ya kwanza ya ujenzi wake inagharimu kiasi cha shilingi Bilioni 165 ni moja ya mkakati wa Serikali katika kuboresha na kuimarisha usafiri wa anga, ambapo kiwanja hicho kitakuwa na uwezo wa kupokea abiria Milioni 1.5 kwa mwaka na abiria 800 kwa wakati mmoja.







*Muonekano wa hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, jijini Dodoma. Ujenzi wa barabara hiyo hadi sasa umefikia asilimia 36.*

# SERIKALI KUJENGA KWA LAMI BARABARA UNGANISHI MBEYA NA SONGWE

Na **Shukuru Senkondo**



*Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kalembo wilayani Ileje lipokagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Ibungu-Kalembo-Katengele-Kafwafwa KM 46.4 inayounganisha wilaya ya Ileje na Rungwe ambayo ujenzi wake katika maeneo korofi unaendelea kwa kiwango cha changarawe na zege.*

Serikali imesema barabara zote za kimkakati zinazounganisha mikoa ya Mbeya na Songwe zitajengwa kwa kiwango cha lami ili kuufungua ukanda wote wa kusini magharibi mwa Tanzania kwa lami.

Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya amesema katika kuhakikisha hilo tayari Serikali imetoa zaidi ya shilingi milioni 800 ili kuwalipa fidia wananchi watakaoguswa na ujenzi wa barabara ya Isongole-Ndembo hadi Isoko km 52.14 inayounganisha wilaya za Ileje na Kyela.

"Maeneo haya licha ya uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula, miti na uvuvi pia ni maeneo ya mipakani yanayohitaji barabara za uhakika zinazoweza kupitika kipindi chote cha mwaka ", amesisitiza Eng. Kasekenya.

Amezungumzia umuhimu wa wananchi waliolipwa fidia kupisha maeneo ya barabara ili mkandarasi kuanza kazi mapema iwezekanavyo.

"Kama umelipwa fidia ni vizuri ukatafuta eneo jingine ili kuiwezesha Serikali kumkabidhi mkandarasi eneo la mradi na kazi ya ujenzi ianze mara moja," amesema Naibu Waziri huyo wa ujenzi.

Kuunganika kwa barabara za mkoa wa Songwe na Mbeya kutarahisisha shughuli za uchukuzi na usafiri mipakani na hivyo kuchochea ufanisi katika mipaka na kuwavutia wasafirishaji wengi kutumia bandari za Tanzania.

Amesema kukamilika kwa kiwango cha lami kwa barabara za Mlowo-Kamsamba, Mbalizi-Mkwajuni-Makongolosi, Isongole-Ndembo –Isoko, Ibungu –Kalembo-Katengele-Kafwafwa-Kiwira-Kimo na Igawa-Mbeya-Tunduma kutachochea ukuaji mkubwa wa uchumi wa mikoa ya nyanda za juu kusini na magharibi mwa nchi.



*Muonekano wa barabara ya Ibungu-Kalembo-Katengele-Kafwafwa KM 46.4 inayounganisha wilaya ya Ileje na Rungwe ambayo ujenzi wake katika maeneo korofi unaendelea kwa kiwango cha changarawe na zege wilayani Ileje.*

# AGIZO LA BASHUNGWA UVAAJI VIFAA VYA USALAMA LATEKELEZWA

Na **Sandra Kiwia**



*Mfanyakazi wa Kampuni ya kikandarasi ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCEC) akiendelea na hatua ya ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje, jijini Dodoma (Dodoma Outer Ring Road) huku akiwa amevaa vifaa vya usalama mahala pakazi, tarehe 3 Oktoba ,2023.*

Wakala wa Barabara (TANROADS) jijini Dodoma, umesema kuwa utahakikisha unaendelea kusimamia utekelezaji wa masuala ya usalama kwa wafanyakazi wanaotekeleza miradi ya Sekta ya Ujenzi katika miradi yote nchini.

Hayo yamesemwa na Mhandisi Alinanuswe Mwakiluma, kwa niaba ya Meneja wa TANROADS mkoa wa Dodoma, Mha. Leonard Chimagu, leo tarehe 3 Oktoba, 2023 jijini humo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na agizo la Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alilolitoa wakati alipotembelea mradi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje (Km 112.3) jijini humo tarehe 29 Septemba, 2023 kwa Mkandarasi China Civil Engineering Construction Corporation (CCEC) na kukuta baadhi ya wafanyakazi wamevaa viatu vilivyochanika.

Mhandisi Mwakiluma, amesema kuwa jukumu la Wakala huo ni kuhakikisha kuwa kila mfanyakazi anapatiwa vifaa mbalimbali vya usalama kwa mujibu wa mkataba ili kumlinda wakati wa changamoto yoyote inapoweza kujitokeza mahala pakazi.

"Nadhani mmeshuhudia wenyewe, wafanyakazi wa Mkandarasi huyu tayari wamepewa vifaa vya usalama ikiwemo kofia ngumu, viatu, barakoa na kiakisi mwanga (reflector), kwa hiyo sisi kama TANROADS mtaona ni namna gani tulivyoweza kufuatilia na kutekeleza agizo la Waziri, amesema Mha. Mwakiluma.

Ameongeza kuwa TANROADS itahakikisha inaendelea kutekeleza maelekezo ya Waziri huyo kuhusiana na suala hilo hata kwa makandarasi wengine wanaoendelea kutekeleza miradi ya ujenzi katika maeneo mbalimbali nchini.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Mkandarasi kutoka kampuni ya CCEC, Mha. David Kapinga, amesema kuwa jumla ya vifaa 50 vimebadilishwa, na kampuni yao imekuwa ikigawa vifaa vya usalama kila baada ya miezi mitatu ila baada ya agizo la Waziri Bashungwa kwa sasa utaratibu utabadilishwa na kugawa vifaa vingine mara tu vya awali vitakapokuwa vimeharibika.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, akiangalia kiatu cha mmoja wa Wafanyakazi katika mradi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje ya Dodoma yenye urefu wa kilometa 112.3; sehemu ya Nala -Veyula – Mtumba (km 52.3), Septemba 29, 2023 jijini Dodoma. Amemsisitiza Mkandarasi China Civil Engineering Corporation kuwanunulia vifaa vya usalama wafanyakazi wake.



Mfanyakazi wa Kampuni ya kikandarasi ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCEC) akiendelea na hatua ya ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje, jijini Dodoma (Dodoma Outer Ring Road) huku akiwa amevaa vifaa vya usalama mahala pakazi, tarehe 3 Oktoba ,2023.



Naye, Innocent Isaka, akizungumza kwa niaba ya Wafanyakazi wa Kampuni ya kikandarasi ya CCEC amesisitiza kwa wakandarasi kuendelea kutoa vifaa kwa wafanyakazi pindi vinapoharibika na kutoa rai kwa wafanyakazi kuwa waaminifu na kuvitunza vifaa hivyo ambavyo vinapunguza vihatarishi katika maeneo ya kazi.

Tamimu Budi, ameishukuru kampuni yao kwa kuweza kutekeleza agizo la Waziri kwa wakati na amesisitiza kuendelea kufanya hivyo kwani vifaa hivyo vinawapa hamasa na utambuzi hata wakati wa usiku

Mradi wa Barabara ya Mzunguko wa nje ya Dodoma (Km 112.3), unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa gharama ya shilingi Bilioni 221 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2024.

# BILIONI 60.1 KUKARABATI KIWANJA CHA NDEGE CHA SUMBAWANGA

Na **Shukuru Senkondo**



*Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya akisisitiza jambo kwa Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Rukwa Eng. Mgeni Mwanga alipokagua barabara ya Matai-Tatanda KM 25 mkoani Rukwa.*

Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya amesema zaidi ya shilingi bilioni 60.1 zinatarajiwa kutumika katika ukarabati na uboreshaji wa kiwanja cha ndege cha Sumbawanga.

Amesema hatua hiyo ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuimarisha usafiri wa anga nchini na kuwezesha maeneo mengi ya nchi kufikika kwa njia ya anga ambapo viwanja vinne vya Tabora, Kigoma, Sumbawanga na Shinyanga vinajengwa,

Akizungumza na wakazi wa Manispaa ya Sumbawanga Eng. Kasekenya amewataka kutoa ushirikiano kwa mkandarasi M/s Beijing Construction Engineering Group Co. Ltd ili akamilishe ujenzi huo kwa wakati.

"Tunatarajia ifikapo Machi 2025 kazi ya ukarabati na upanuzi wa kiwanja hiki katika njia ya kuruka na kutua ndege yenye urefu wa kilomita 1.750m, barabara za maungio na maegesho ya ndege, jengo la abiria, taa za kuongozea ndege na uzio wa usalama katika kiwanja hicho view vimekamilika", amesema Eng. Kasekenya.

Amezungumzia umuhimu wa wakazi wa mkoa wa Rukwa kuhakikisha wanatumia fursa za uwepo wa miundombinu ya kisasa kujiletea maendeleo.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri huyo wa Ujenzi amekagua na kuelezea kuridhishwa kwake na kazi ya ujenzi wa barabara za Ntendo-Kizungu KM 25 ambayo ni sehemu ya barabara ya Ntendo-Muze-Kilyamatundu KM 179 na barabara ya Matai – Tatanda KM 25 ambayo ni sehemu ya barabara ya Matai-Kisesya KM 50 na kusisitiza kuwa nia ya Serikali ni kuzijenga barabara hizo zote kwa lami ili kuhuisha huduma za usafiri na uchukuzi na kuongeza biashara ya mazao katika ukanda wa Magharibi.

"Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anatoa fedha nyingi kujenga barabara hizi, njia bora ya kumuunga mkono ni kuongeza uzalishaji wa mazao na kuilinda miundombinu hii kwa wivu mkubwa", amesisitiza Naibu Waziri huyo.

Amewataka wakandarasi wote mkoani Rukwa kufanyakazi kwa kuzingatia muda, ubora na utabiri wa hali ya hewa ili kazi zisikwame na huduma za usafiri na uchukuzi zisisimame.

Naibu Waziri Kasekenya anaendelea na ziara yake ya kukagua ujenzi wa miundombinu katika kanda ya magharibi inayohusisha mikoa ya Tabora,Kigoma,Katavi na Rukwa.



*Naibu Waziri wa Ujenzi Eng. Godfrey Kasekenya akisisitiza jambo kwa Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Rukwa Eng. Mgeni Mwanga alipokagua barabara ya Matai-Tatanda KM 25 mkoani Rukwa.*



*Muonekano wa daraja la Mlokola na barabara ya Laela-Mwimbi-Kasesya ambayo ujenzi wake kwa kiwango cha lami unaendelea mkoani Rukwa.*

# KASEKENYA AIASA AQRB KUIMARISHA USHIRIKIANO KAZINI

Na **Neema Macha**




*Naibu waziri wa Ujenzi Mteule, Mha.Godfrey Kasekenya akifafanua jambo wakati wa Ufunguzi wa Mkutano wa kikao cha faragha cha wafanyakazi wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Jijini Dodoma.*

Naibu Waziri wa Ujenzi Mteule, Mha. Godfrey Kasekenya amewataka watumishi wa Bodi ya Usajili Wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi Nchini (AQRB) kufanya kazi kwa ushirikiano na kutatua changamoto zao katika maeneo yao ya kazi ili kuongeza weledi kwenye utendaji.

Ameyasema hayo alipokua akifungua kikao cha wafanyakazi wa Bodi hiyo, kilichofanyika katika Ukumbi wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Jijini Dodoma, ambapo ameeleza miongoni mwa manufaa ya ushirikiano na umoja kazini ni pamoja na kuifanya taasisi kutoa huduma za viwango kwa wadau.

"Vikao kama hivi vinasaidia watu kuondokana na mazingira ya utendaji ya kawaida sababu mnakaa pamoja mnafahamiana vizuri kitabia, mnajitathmini na kuja na suluhu ya utatuzi wa changamoto ambazo zinakabili taasisi maana vinahusisha kila kada zote, tumieni vizuri fursa hii" amesema Kasekenya.

Akifafanua umuhimu wa kikao hicho Mha, Kasekenya amewataka watumishi wa bodi hiyo kuacha kufanya kazi kwa mazoea kwani mazingira ya utendaji wa taasisi ni kutoa huduma kwa watalaam wa fani ya wabunifu majengo na wakadiriaji wa majenzi.

Aidha Naibu Waziri wa ujenzi Mteule, Mha Godfrey Kasekenya, amesema Serikali inathamini mchango wa AQRB na inahitaji michango ya bodi katika kuwezesha na kuendelea ujenzi wa Tanzania ya viwanda kwa kusisitiza kuwepo kwa mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu wake ili wapate uzoefu na ujuzi hatimaye waweze kushindana katika soko la ndani na nje ya nchi.

Kwa upande wa Naibu Katibu Mkuu, Bwa. Ludovick Nduhiye, amewapongeza AQRB kwa kuendelea kufanya vikao vya wafanyakazi na kuwataka watumishi kuhakikisha wanaeleza kwa uwazi changamoto zote wanazokutana nazo ili kuimarisha utendaji wa taasisi.

“Kama watumishi wa Ummamna wajibu mkubwa katika kuhakikisha majenzi yanafata viwango vinavyotakiwa kulingana na fani inavyotaka, kama wataalamu serikali inawategemea sana kwenye ushauri hususani katika kipindi hiki ambacho taasisi na wananchi wanajenga sana mji wa Dodoma”alisisitiza Bwa. Nduhije.

Naye Msajili wa Bodi Arch. Edwin John Nnunduma amesema dhumuni la mkutano huo ni kujadili na kufikia muafaka kwenye maamuzi yanayohusu maslahi ya watumishi na watendaji kazi wenye tija kwa maendeleo ya bodi na taifa.



*Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi Mteule , Bwa. Ludovick Nduhiye akizungumza kwenye kikao cha faragha cha wafanyakazi wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB) kilichofanyika katika ukumbi wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) , jijini Dodoma.*



*Naibu Waziri wa Ujenzi Mteule, Mha. Godfrey Kasekenya (katikati ,waliokaa wakiwa) , na Naibu Katibu Mkuu Mteule, Bwa. Ludovick Nduhije ( wa Pili kulia waliokaa) wakiwa kwenye picha ya pamoja na Msajili wa Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Arch. Edwin John Nnunduma ( wa pili kushoto) pamoja na wajumbe kutoka Chama cha Wafanyakazi (TAMICO – AQRB), mara baada ya Ufunguzi wa kikao cha faragha cha wafanyakazi kilichofanyika Jijini Dodoma.*

# UBORA WA VIFAA VINAVYOTUMIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI NCHINI UNAZINGATIWA

Na **Siti Said**



*Mafundi wakiendela na kazi ya Ujenzi wa moja ya kalvati kwenye Barabara ya mzunguko wa nje wa jiji la Dodoma ( Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road), yenye jumla ya kilomita 112.3. ambapo ujenzi wake unatarajiwa kukamilika Disemba 2024.*

Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), umewatoa hofu Watanzania kuhusu ubora wa vifaa vinavyotumika katika utekelezaji wa miradi inayoendelea nchini ikisema ni imara na bora.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Mohamed Besta, alitoa ufafanuzi huo jana mkoani Dodoma baada ya kufanya ziara ya ukaguzi katika maabara inayotumika kupima viwango na ubora wa vifaa.

Pia alifanya ukaguzi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje katika wa Jiji la Dodoma sehemu ya pili, kutoka Nala-Veyula-Mtumba (Km 52.3) ambayo hadi sasa ujenzi wake umefikia asilimia 51.

Wakati wa ukaguzi huo, Mhandisi Besta, aliwataka wataalamu hao kuhakikisha kuwa vifaa vyote vya ujenzi ikiwemo nondo, kokoto, udongo vinapimwa kwa weledi kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa katika utekelezaji wa mradi.

“Serikali inatumia fedha nyingi katika utekelezaji wa miradi yake, hivyo wataalam ambao mmeaminiwa kusimamia miradi hii pamoja na mshauri mwelekezi hakikisheni mnapima malighafi zote za ujenzi na endapo mtakuta hazikidhi vigezo visitumike katika mradi wowote,” alisema Mhandisi Besta.

Aidha, Mhandisi Besta alisema katika kuhakikisha ubora na viwango vya ujenzi vinazingatiwa wanaendelea kufuatilia upimaji wa malighafi zote zinazotumika katika miradi yote inayosimamiwa na TANROADS ili kuhakikisha barabara na madaraja yanayojengwa yanadumu na kukidhi thamani ya fedha.

“Miradi yote iliyopo chini ya TANROADS inafuatiliwa kwa umakini na ubora kulingana na thamani ya fedha ambayo imewekwa” alisema Mhandisi Besta.

Naye Mhandisi wa vifaa, anayesimamia mradi wa barabara ya mzunguko wa nje jijini Dodoma, Mhandisi Deogratius Nyambo alisema kuwa vifaa vyote kabla havijaanza kutumika huingizwa katika maabara kwa ajili ya kupimwa ubora na endapo vitabainika havijakidhi huondolewa sehemu ya mradi.

Alisema katika kusimamia ubora kuna kazi za kila siku zinazofanyika ikiwamo kupima ubora wa udongo, tabaka la tuta la barabara kulingana na viwango vilivyowekwa vya mradi husika ili kuhakikisha barabara na madaraja zinadumu kwa muda mrefu.

Barabara ya mzunguko wa nje wa Jiji la Dodoma (Km 112.3) ambayo ujenzi wake umegawanywa katika sehemu mbili, ambazo ni Nala-Veyula-Mtumba (Km 52.3) pamoja na Ihumwa-Matumbulu-Nala (Km 60) unatarajiwa kukamilika Desemba mwakani, ambapo pamoja na mambo mengine itapunguza msongamano katika jijini Dodoma na kuchochea shughuli za kiuchumi.




*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Mhandisi Mohamed Besta, akizungumza na waandishi wa Habari mara baada ya kukagua Maabara inayotumika kupima viwango na ubora vinavyotumika katika ujenzi wa barabara ya Mzunguko wa Nje wa Jiji la Dodoma.*



*Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Mhandisi Mohamed Besta, akimsikiliza Kaimu Meneja wa Wakala wa barabara Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Salehe Juma wakati alipotembelea na kukagua Maabara inayotumika kupima viwango na ubora wa vifaa pamoja na kutembelea barabara ya Mzunguko wa Nje wa Jiji la Dodoma.*

# MENEJIMENTI YA SEKTA YA UJENZI YAKAGUA JENGO LA WIZARA, MTUMBA JIJINI DODOMA

Na **Christina Seggu**











*Sehemu ya menejimenti ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), wakikagua maendeleo ya ujenzi wa jengo jipya la Ofisi la Wizara hiyo, eneo la Mtumba, jijini Dodoma.*


MV.KAZI
SEATAXI


SOON
HOME
WCF


Karibu MAGOMENI KOTA

**Wizara ya Ujenzi,**
**Mji wa Serikali Mtumba,**
**S.L.P 2888**
**DODOMA.**

**Simu: +255 26 23244455 / +255 26 2322703, 2322702**
**Nukushi: +255 26 2323233 / +255 26 2322704**
**Barua pepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mow.go.tz**

#KAZIIENDELEE